

11A-Makhaarij Al-Huruwf (Matokeo Ya Herufi) - Al-Jawf (Uwazi Wa Kinywa)

1. الجؤف Al-Jawf - Uwazi Wa Kinywa¹

Katika sehemu hii ya uwazi wa kinywa kunapatikana makhraj moja tu ambamo hutoka herufi tatu za madd; nazo ni:

| | | |
|------|---|--|
| Alif | ا | Iliyo na sukuwn na kabla yake kuna fat-hah inatamkwa 'aa' |
| Waw | و | Iliyo na sukuwn na kabla yake kuna dhwammah inatamkwa 'uw' |
| Yaa | ي | Iliyo na sukuwn na kabla yake kuna kasrah inatamkwa 'iy' |

Wakati wowote ule herufi hizi tatu zikiwa hazifungamani na sharti hizo zilizotajwa basi huwa na matokeo mengine kwani wakati huo huwa si herufi za madd. Na herufi tatu hizi zimekusanyika katika kauli ya Allaah: نُوحِيهَا (nuwhiyhaa)

¹Herufi hizi juu ya kuitwa kuwa ni herufi za Jawfi; pia hueleweka kama ni herufi za maddiyah (za madd) na herufi za hawaaiyyah (herufi za hewa)